

# **CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA**



## **MWONGOZO WA ULINZI NA USALAMA**

**AGOSTI 2023**

## **DIBAJI**

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kina wajibu wa kuhakikisha kivitendo na bila shaka uwepo wa usalama na mazingira ambayo hakuna vitendo vya uhalifu na au vya kijinai kwa wanajamii wote.

Chuo kinalenga kupunguza na kuondoa hatari zote kwa jamii yake na mali zake kwa kuhakikisha kunakuwepo uongozi bora ambapo usimamizi wa ulinzi na usalama wa wanajamii na mali za Chuo unatekelezwa katika ngazi zote za utawala.

Kwa msingi huo, ulinzi wa Chuo, jamii na mali zake unategemea sana mchango wa kila mdau kwa kuamini kuwa suala la ulinzi na usalama ni shirikishi na ni wajibu wa kila mmoja wetu.

Aidha, uwepo wa mazingira salama kwa Chuo chetu, jamii na mali zake kutawezesha sisi kama Taasisi kujikita katika utekelezaji wa mikakati yetu na kuleta maendeleo tarajiwa kwa Chuo chetu na taifa kwa ujumla.

Kwa niaba ya Chuo, ninawashukuru nyote mlioshiriki kwa namna mbalimbali na pia nawashurukuru wadau wote kwa michango yao iliyofanikisha kuandaa mwongozo huu.

Prof. Aloys N. Mvuma

**MAKAMU MKUU WA CHUO**

**CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA**

## **YALIYOMO**

DIBAJI.....	i
TAFSIRI YA MANENO YALIYOTUMIKA.....	iv
VIFUPISHO .....	vi
1.0 UTANGULIZI .....	1
1.1 Historia ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya.....	1
1.2 Lengo Kuu.....	2
1.2.1 Malengo mahsusi .....	2
1.3 Eneo / Mawanda ya mwongozo .....	2
1.4 Mapitio ya Mwongozo .....	3
2.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO .....	1
2.1 Kamati ya Ulinzi na Usalama.....	1
2.1.1 Majukumu ya Kamati ya Ulinzi na Usalama.....	2
2.2 Wasimamizi wa Mwongozo.....	3
2.2.1 Menejimenti ya Chuo.....	3
2.2.2 Wadau na majukumu yao .....	3
3.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YAHUSUYO ULINZI NA USALAMA.....	5
3.1. Muundo wa Ofisi ya Ulinzi na Usalama .....	5
3.2. Mchakato wa kupata Kampuni ya Ulinzi.....	5
3.3. Biashara Ndani ya Eneo la Chuo .....	6

3.4	Utaratibu wa Kuingiza au Kutoka Mali Ndani ya Eneo la Chuo .....	6
3.5	Kubaini Muhalifu/Uhalifu na Uwajibikaji Unapotokea Uhalifu.....	9
3.6	Taarifa kwa Ofisi ya Ulinzi na Usalama.....	11
3.7	Kuzuia au kupunguza matukio ya uhalifu .....	11
3.8	Utunzaji wa Funguo za Ofisi .....	12
3.9	Matumizi ya Mawasiliano .....	13
3.10	Adhabu kwa Makosa Mbalimbali .....	13
3.11	Ujirani Mwema .....	14
3.12	Matumizi ya Mifumo ya Kamera za Usalama (CCTV) na Usalama wa Mifumo ya Taarifa .....	14
3.13	Ushughulikiaji wa Madawa ya Kulevya .....	15
3.14	Udhibiti wa Silaha na Vifaa vya Milipuko .....	16
3.15	Udhibiti wa Kemikali na Vifaa Vingine Vinavyoweza Kuathiri Usalama 16	
4.0	UFUATILIAJI NA TATHMINI.....	17
4.1.	Mbinu za Ufuatiliaji.....	17
4.2.	Vifaa vya Ufuatiliaji .....	18
	VIAMBATANISHO.....	19
	UTHIBITISHO .....	23

## **TAFSIRI YA MANENO YALIYOTUMIKA**

Biashara	Shughuli au mchakato wowote ule ulio halali unaofanywa kwa lengo la kutengeneza faida
Chuo	Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya
Eneo la Chuo	Eneo lililopimwa na linalomilikiwa kisheria na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya
Jumuiya ya MUST	Watu wanaoishi au kufanya shughuli ndani ya eneo la Chuo
Jamii jirani	Wale wanaoishi katika vijiji au mitaa inayopakana na eneo la Chuo
Kampuni ya ulinzi	Taasisi ya ulinzi inayotoa huduma ya ulinzi na usalama katika enea la Chuo
Mdau	Mtu mwenye maslahi na Chuo
Menejimenti	Chombo cha maamuzi cha Chuo
MUST Charter	Hati idhini/makubaliano ya kuundwa kwa Chuo
Mkataba	Ni makubaliano kati ya pande mbili tofauti na kufuata misingi ya sheria ya nchi na usiwe wa kulazimishwa upande wowote ule
Mwanachuo	Mtu yeyote aliyesajiliwa na anayehudhuria masomo ya Chuo
Ulinzi	Kuzuia viashiria vya uhalifu na uhalifu wenyewe

Usalama

Hali ya kutokuwepo kwa viashiria vya uhalifu na  
uhalifu wenyewe

## **VIFUPISHO**

AHRMC	Administration and Human Resource Management Committee
CEMC	Contract Execution and Monitoring Committee
CCTV	Closed Circuit Television
JKT	Jeshi la Kujenga Taifa
JWTZ	Jeshi la Wananchi wa Tanzania
MIST	Mbeya Institute of Science and Technology
MTC	Mbeya Technical College
MUST	Mbeya University of Science and Technology
MUSTASA	Mbeya University of Science and Technology Academic Staff Association
NACTE	National Council for Technical Education
PPA	Public Procurement Act
PPR	Public Procurement Regulations
PPRA	Public Procurement Regulatory Authority
RAAWU	Researchers Academician and Allied Workers Union
TBS	Tanzania Bureau of Standards
THTU	Tanzania Higher Learning Institutions Trade Union

## **1.0 UTANGULIZI**

Mwongozo huu utazingatia miongozo ya Ulinzi na Usalama wa Nchi. Ulinzi na usalama ni msingi mkubwa wa maendeleo ya jamii katika ngazi zote, na kwa hakika hakuna jamii yoyote ambayo itajivunia kupata muelekeo wa maendeleo kama hakuna uhakika wa ulinzi na usalama kwao na mali zao. Katika kutekeleza hili, ni wajibu wa kila Mwananchi kushiriki kikamilifu kuhakikisha ulinzi na usalama unakuwepo. Jambo hili litawezekana kama kila mmoja wetu atakuwa na nia ya dhati na kuwa na miongozo na ufuatiliaji thabiti wa namna bora ya kudumisha ulinzi na usalama.

Mwongozo huu wa Ulinzi na Usalama wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya umeundwa kwa kuzingatia kuwa Chuo kinakua na kutanuka kwa msingi wa kuongezeka kwa wafanyakazi, Wanachuo na jamii inayozunguka Chuo pamoja na kuongezeka kwa majukumu yanayofanywa na Chuo.

Mwongozo huu utasaidia kuweka namna bora ya kulinda na kuhifadhi mazingira ikiwemo uoto wa asili unaozunguka eneo la Chuo. Pia, Mwongozo huu unaainisha namna ya mahusiano ya Chuo na jamii inayozunguka.

### **1.1 Historia ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

Historia ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ilianza mwaka 1986 wakati huo kikijulikana kama Chuo cha Ufundi Mbeya (*Mbeya Technical College - MTC*) kilipoanzishwa kwa ajili ya kutoa programu za *Vyeti vya ufundi Sanifu*. Julai, 2005, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*National Council fo Technical Education - NACTE*) lilikipandisha hadhi MTC kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (*Mbeya Institute of Science and Technology - MIST*) kwa Sheria Na. 9 ya mwaka 1997. Baada ya mabadiliko hayo, MIST ilianza kutoa kozi mbalimbali. MIST ilibadilishwa hadhi na kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (*Mbeya University of Science and Technology - MUST*) kwa



Sheria Na. 7 ya mwaka 2005 na Hati Idhini ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ya Mwaka 2013.

## **1.2 Lengo Kuu**

### **1.2.1 Malengo mahsusi**

Malengo ya Mwongozo huu ni kama ifuatavyo:

- (a) Kuongeza ufanisi katika utendaji wa shughuli za ulinzi na usalama;
- (b) Kuongeza ushiriki wa Ofisi ya Ulinzi na Usalama ya Chuo kuratibu mali za Taasisi au wadau zinapoingizwa au kutolewa nje ya Taasisi;
- (c) Kupata taarifa ya kuingia na kutoka kwa wageni mbalimbali wa Taasisi;
- (d) Ushirikishwaji wa Ofisi ya Ulinzi na Usalama katika maamuzi yahasuyo ulinzi na usalama wa Chuo mfano, katika mchakato wa kupata kampuni za ulinzi;
- (e) Kusaidia Ofisi ya Ulinzi na Usalama kupata taarifa rasmi za maamuzi ya vikao mbalimbali zinazohusu ulinzi na usalama;
- (f) Kuzuia kuuza au kuzunguka na bidhaa bila kuwa na kibali cha Taasisi mfano, kuuza vyakula mbalimbali au nguo.
- (g) Kuzuia shughuli zinazo athiri mazingira ya Chuo bila kibali mfano, kukata miti, kuchunga au kukata majani ya mifugo; na
- (h) Kuelimisha na kuhamasisha jamii kuwa jukumu la ulinzi ni la kila mwanajamii.

## **1.3 Eneo / Mawanda ya mwongozo**

Mongozo huu utawahusu:

- (a) Wafanyakazi wote;
- (b) Wanachuo wote;
- (c) Kampuni za ulinzi;

- (d) Jamii inayozunguka Chuo; na
- (e) Wageni wote wa MUST.

#### **1.4 Mapitio ya Mwongozo**

Marekebisho yoyote juu ya Mwongozo huu yataamuliwa na Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya na kuidhinishwa na Kamati ya Ajira, Utumishi na Raslimaliwatu kila baada ya miaka mitatu (3) au muda wowote kwa kutegemea na mahitaji ya wadau kama walivyoorodheshwa na mwongozo huu.

## **2.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO**

Kupanuka kwa Chuo kuna faida nyingi kwa jamii nzima ndani na nje mathalani, kuongeza ajira kwa Wafanyakazi, kuongeza udahili wa Wanachuo na kuongezeka kwa muingiliano baina wa wadau. Pamoja na faida hizo, upanuzi huo una changamoto kadhaa zinazoweza kujitokeza zinazosababishwa na muingiliano kijamii mfano kuongezeka kwa biashara kusikofuata utaratibu. Kwa muktadha huo, ni dhahiri kuwa mabadiliko ya tabia na kuongezeka kwa matukio yanayohatarisha ulinzi na usalama, mfano; kuongezeka kwa wafanyabiashara wasio na vibali, ukataji wa miti, uporaji na utumiaji wa dawa za kulevya na muingiliano na jamii inayozunguka Chuo usio rasmi yameongezeka.

Kwa kutambua hilo, Chuo kimeona ni wakati muafaka kuwa na mwongozo utakaoelekeza juu ya mambo kadha wa kadha yahusuyo ulinzi na usalama wa wafanyakazi na jamaa zao, mali zake na jamii inayozunguka ili kuwa na jamii yenye amani na shirikishi.

### **2.1 Kamati ya Ulinzi na Usalama**

Kutakuwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama itakayokuwa na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa jumla wa mwongozo huu. Kamati hii itaundwa na:

- |   |         |
|---|---------|
| (a) Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango Fedha na Utawala - Mwenyekiti |         |
| (b) Mkuu wa Idara ya Ulinzi na Usalama                              | Katibu  |
| (c) Mkurugenzi wa Menejimenti ya Miliki                             | Mjumbe  |
| (d) Mkurugenzi wa Huduma za Wanachuo                                | Mjumbe  |
| (e) Mwanasheria wa Chuo   | Mjumbe  |
| (f) Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu                         | Mjumbe  |
| (g) Wenyeviti na Maafisa watendaji wa mitaa                         | Wajumbe |

(Ikuti, Inyala, Sisitila, Swaya, Lupeta)

- |  |         |
|--|---------|
| (h) Waziri wa Ulinzi wa Serikali ya Wanachuo     | Mjumbe  |
| (i) Mkuu wa Kituo cha Polisi kilicho jirani      | Mjumbe  |
| (j) Mwakilishi mmoja toka THTU, RAAWU na MUSTASA | Wajumbe |

### **2.1.1 Majukumu ya Kamati ya Ulinzi na Usalama**

Kamati ya Ulinzi na Usalama itakuwa na majukumu yafuatayo:

- (a) Kuunda, kuanzisha na kusimamia misingi mikuu ya ulinzi na usalama wa Chuo kwa ajili ya kulinda maslahi ya Chuo, wafanyakazi, wanachuo na jamii kwa ujumla;
- (b) Kufanya mapitio ya Sera ya Ulinzi na Usalama na mambo mengine yanayohusiana na ulinzi na usalama;
- (c) Kufanya tathmini ya muda mfupi na mrefu juu ya hali ya usalama wa Chuo na kupendekeza hatua stahiki za kuchukuliwa;
- (d) Kupokea na kuchambua ripoti ya hali ya ulinzi na usalama wa Chuo kutoka kwa wasimamizi mfano, Serikali ya Wanachuo, Idara ya Ulinzi na Usalama na Kamati ya kusimamia Utekelezaji wa mikataba (CEMC) kutoa maelekezo sahihi;
- (e) Kuhakikisha Mwongozo wa Ulinzi na Usalama inawafikia walengwa;
- (f) Kutoa elimu kwa walengwa juu ya Mwongozo wa Ulinzi na Usalama;
- (g) Kushughulikia mashauri yahasuyo uvunjifu wa ulinzi na usalama kwa kampuni ya ulinzi, taasisi au mtu yeyote na kushauri hatua stahiki;
- (h) Kufanya kazi zingine zinazohusu ulinzi na usalama kama itakavyoelekezwa na Menejimenti ya Chuo; na
- (i) Kamati ya Ulinzi na Usalama itawajibika kwa Kamati ya Utawala na Menejimenti Rasiliamali Watu na itafuata utaratibu wa vikao kama utakavyopangwa na Menejimenti.

## **2.2 Wasimamizi wa Mwongozo**

### **2.2.1 Menejimenti ya Chuo**

Menejimenti ya Chuo ina mamlaka ya kuidhinisha, kusimamia utekelezaji, kufanya tathmini na kutoa mapendekezo au maagizo kwa wadau wote juu ya namna bora ya kutekeleza Mwongozo huu.

#### **2.2.1.1 Makamu Mkuu wa Chuo**

Makamu Mkuu wa Chuo atakuwa kiongozi mkuu katika utekelezaji wa mwongozo huu na atawajibika kuripoti kwa vyombo vya juu mambo yote yanayohusu hali ya ulinzi na usalama wa Chuo.

#### **2.2.1.2 Baraza la Wafanyakazi la Chuo**

Chombo hiki kitakuwa na wajibu wa kujadili ripoti mbalimbali, kuishauri Menejimenti namna bora ya kutekeleza Mwongozo huu na kubuni mikakati ya kuboresha hali ya ulinzi na usalama wa Chuo.

### **2.2.2 Wadau na majukumu yao**

#### **2.2.2.1 Wadau**

Wadau wafuatao watahusika katika utekelezaji wa Mwongozo huu, wadau hawa ni pamoja na:

- (a) Wanachuo wa MUST
- (b) Jamii Jirani ya MUST
- (c) Wafanyakazi wa MUST;
- (d) Kampuni ya ulinzi wa Chuo;
- (e) Kampuni zenye mikataba ya kutoa huduma ndani ya Chuo;
- (f) Vyombo vya kisheria vya ulinzi na usalama Nchini; na

- (g) Mtu au taasisi yoyote ambayo kwa namna moja au nyingine ina uhusiano na Chuo.

#### **2.2.2.2 Wajibu wa wadau**


Wadau ambao wameainishwa au kutoainishwa na Mwongozo watakua na wajibu ufuatao katika kutekeleza Mwongozo huu:

- (a) Kutoa taarifa kwa kampuni ya ulinzi, Ofisi ya Ulinzi na Usalama au katika chombo kingine cha usalama juu ya tukio lolote lililotokea au ambalo linaweza kutokea;
- (b) Kushiriki kutoa maoni ya namna bora ya kuzuia uhalifu;
- (c) Kushirikiana na wadau wengine kutoa elimu juu ya viashiria vya uhalifu;
- (d) Kutoa ushirikiano inapotakiwa; na
- (e) Kuelimisha na kuhamasisha jamii swala la ulinzi na usalama kuwa ni la kila mwanajamii.

### 3.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YAHUSUYO ULINZI NA USALAMA

#### 3.1. Muundo wa Ofisi ya Ulinzi na Usalama

Ili kuboresha Ulinzi na Usalama wa Chuo, Ofisi ya Ulinzi na Usalama itakuwa na muundo ufuatao:



#### 3.2. Mchakato wa kupata Kampuni ya Ulinzi

Ili kupata kampuni bora ya ulinzi na usalama Chuo kitazingatia mambo yafuatayo:

- (a) Mchakato wa upatikanaji wa kampuni za utoaji wa huduma ya ulinzi na usalama utazingatia sheria na kanuni za Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (*Public Procurement Regulatory Authority - PPRA*) na taratibu zilizowekwa na Chuo; na
- (b) Ushirikishwaji mpana wa wadau wenye uzoefu katika tasnia ya ulinzi na usalama kama vile Jesho la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Polisi utazingatia sheria ya Manunuzi ya Umma (PPA) na kanuni zake (PPR) na taratibu zilizowekwa na Chuo.

### **3.3. Biashara Ndani ya Eneo la Chuo**

- (a) Ni makosa kwa wafanyakazi, wanachuo au mtu yeyote kufanya biashara ndani ya eneo la Chuo bila kufuata taratibu zilizowekwa na Chuo. Lengo ni kuzuia muingiliano ambao unaweza kuhatarisha usalama wa nyaraka na taarifa mbalimbali. Zuoio hili pia lina lengo la kuongeza uwajibikaji na ufanisi katika kazi kwa wafanyakazi husika;
- (b) Chuo kitatoa kibali na mikataba ya kufanya biashara katika eneo la Chuo kwa mtu aliyeomba kwa kufuata utaratibu wa kutuma maombi kwa Makamu Mkuu wa Chuo na kukubaliwa;
- (c) Baada ya mhusika kupewa kibali, atawajibika kusambaza nakala zake katika Ofisi ya Ulinzi na Usalama, kampuni ya ulinzi na Kurugenzi ya Menejimenti ya Miliki kwa kumbukumbu; na
- (d) Chuo kitatenga eneo maalum kwa ajili ya biashara ili kurahisisha shughuli za ulinzi na usalama katika maeneo husika.

### **3.4 Utaratibu wa Kuingiza au Kutoka Mali Ndani ya Eneo la Chuo**

Mdau yeyote anayeingiza au kutoa mali katika eneo la Chuo atazingatia mambo yafuatayo:

- (a) Kuingia mali ndani ya eneo la Chuo:



- (i) Mhusika atatakiwa kutoa taarifa kuhusu mali kwa walinzi wa lango kuu;
  - (ii) Walinzi watakagua nyaraka za mali husika na nakala moja itabaki lango kuu na endapo mhusika hana nyaraka, ataorodhesha mali hizo katika daftari la kumbukumbu la walinzi;
  - (iii) Walinzi watakagua mali husika na kuruhusu uingizwaji wake;
  - (iv) Endapo kutatokea na kutoridhishwa na ukaguzi, walinzi watawasiliana na Ofisi ya Ulinzi na Usalama ya Chuo kwa maelekezo zaidi;
  - (v) Magari binafsi ya wafanyakazi yatatakiwa kuwa na utambulisho utakaobandikwa katika magari yao. Utambulisho huo utatolewa bure na Chuo kupitia Kurugenzi ya Menejimenti ya Miliki;
  - (vi) Wageni wanaoingia katika eneo la Chuo na vyombo vya moto watapewa vitambulisho maalumu na walinzi na kuvirejesha wanapotoka;
  - (vii) Magari ya Serikali yatakaguliwa na kuandikishwa katika daftari la kumbukumbu la walinzi kabla ya kuruhusiwa kuingia au kutoka ndani ya eneo la Chuo isipokuwa ya viongozi waandamizi wa kitaifa yakiwa na viongozi hao;
  - (viii) Kampuni ya ulinzi itawajibika kuangalia usalama wa mali yoyote iliyokaguliwa na kupewa kibali kuingia katika eneo la Chuo;
  - (ix) Wageni wote wanaoingia ndani ya eneo la Chuo watapewa vitambulisho na walinzi katika eneo la mapokezi; na
  - (x) Wageni hao watajiandisha katika daftari na kusainiwa wakati wa kuingia na kutoka wanaporudisha vitambulisho.
- (b) Kutoa mali ndani ya eneo la Chuo kwa kuzingatia ya fuatayo:
- (i) Mali yoyote haitoruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo isipokuwa kwa kibali maalum;

- (ii) Mali hizi zitahusisha kitu chochote ambacho kimetengenezwa au kununuliwa na Chuo au taasisi/mtu binafsi, pamoja na mali yoyote itokanayo na uoto wa asili mfano, miti, nyasi au kitu kingine chochote ambacho Chuo kina manufaa nacho; na
- (iii) Vibali vya mali zisizotokana na uoto wa asili vitatolewa kwa utaratibu ufuatao:

**Hatua ya kwanza:**

Mhusika atajaza fomu kuonyesha aina na idadi ya mali anayotaka kutoa. Fomu hii itatolewa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Menejimenti ya Miliki ya Chuo.

**Hatua ya pili:**

Fomu iliyojazwa na mhusika itapelekwa Ofisi ya Ulinzi na Usalama kwa ajili ya kuthibitishwa.

**Hatua ya tatu:**

Ofisi ya Ulinzi na Usalama itatoa taarifa kwa walinzi wa zamu.

- (iv) Vibali vya mali zinazotokana na uoto wa asili vitatolewa kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:

**Hatua ya kwanza:**

Mhusika atajulisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Menejimenti ya Miliki na atajaza fomu kuonyesha aina na idadi/kiwango cha mali anayotaka kutoa. Fomu hii itatolewa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Menejimenti ya Miliki.

**Hatua ya pili:**

Fomu iliyojazwa na mhusika itapelekwa Ofisi ya Ulinzi na Usalama kwa ajili ya kuthibitishwa.

**Hatua ya tatu:**

Ofisi ya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na Kamati ya Mazingira itapeleka wataalamu kwa ajili ya kufanya tathmini ya gharama ya mali husika.

**Hatua ya nne:**

Mhusika atapatiwa namba ya malipo (*Control Number*) na atalipia gharama hizo benki na kuwasilisha hati ya malipo (*pay-in-slip*) Kurugenzi ya Uhasibu.

**Hatua ya tano:**

Baada ya kujiridhisha na malipo yaliyofanywa, mhusika ataruhusiwa kuvuna mali chini ya uangalizi wa Ofisi ya Ulinzi na Usalama.

**Hatua ya sita:**

Nakala ya Hati ya Malipo itatumika kama kibali cha kutoa mali ndani ya eneo la Chuo.

**3.5 Kubaini Muhalifu/Uhalifu na Uwajibikaji Unapotokea Uhalifu**

Katika kubaini uhalifu au viashiria vya uhalifu, Chuo kwa kushirikiana na wadau wengine watafanya mambo yafuatayo:

- (a) Kuhakikisha Wafanyakazi na Wanachuo wanavaa vitambulisho muda wote wanapokua ndani ya eneo la Chuo. Katika kutekeleza jambo hili, mambo yafuatayo yatazingatiwa:
- (i) Ofisi ya Rasilimaliwatu itasimamia zoezi hili kwa upande wa wafanyakazi na kwa upande wa Wanachuo zoezi litasimamiwa na Ofisi ya Mshauri wa Wanachuo,
  - (ii) Katika kusimamia zoezi hili, walinzi watahakikisha watu wote wanavaa vitambulisho.
- (b) Ofisi ya Ulinzi na Usalama ikishirikiana na Menejimenti ya Chuo itawajibika kufanya mambo yafuatayo:
- (i) Kulinda usalama wa watoa taarifa;
  - (ii) Ofisi ya Ulinzi na Usalama itafanya uhakiki wa taarifa kutoka kwa mtoa taarifa na kuchukua hatua stahiki kulingana na aina ya taarifa;
  - (iii) Kutegemeana na tukio husika, taarifa sahihi zilizohakikiwa zitapelekwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama au Menejimenti kwa hatua zaidi;
  - (iv) Kutegemeana na aina ya uhalifu uliofanyika, Ofisi ya Ulinzi na Usalama itashughulikia uhalifu uliotokea au unaoweza kutokea kwa kuwahusisha wadau au vyombo vingine vya usalama;
  - (v) Kampuni ya ulinzi kwa kushirikiana na Ofisi ya Ulinzi na Usalama ya Chuo na wadau wengine kama Wanachuo na Wafanyakazi wanao wajibu wa kubaini, kuchunguza na kupambana na uhalifu;
  - (vi) Kampuni ya ulinzi itawajibika kukamata, kufungua kesi polisi na mahakamani na kusimamia na kutoa ushahidi pale inapotokea shauri limepelekwa katika vyombo vingine vya ulinzi na usalama; aidha chuo kitashirikiana na Kampuni katika kutoa ushahidi wa tukio lolote la kiusalama endapo litapelekwa katika vyombo vya sheria. Chuo kitalazimika kufungua kesi na kusimamia kesi

ambazo mazingira yake hayahusishi moja kwa moja uwajibikaji wa kampuni ya ulinzi kimkataba; na

- (vii) Endapo kutatokea kushindwa kutimiza majukumu ya ulinzi na usalama kwa kampuni ya ulinzi na kupelekea uhalifu; Chuo na kampuni watatatua mgogoro kwa njia ya mazungumzo kwa mujibu wa mkataba, na njia hii ikishindikana upande wowote utakua na haki ya kupeleka shauri hilo kwenye vyombo vya sheria.

### **3.6 Taarifa kwa Ofisi ya Ulinzi na Usalama**

Katika kutekeleza mwongozo huu Ofisi ya Ulinzi na Usalama itakuwa ndiyo kiungo cha msingi kati ya Menejimenti na wadau. Kwa kuzingatia jukumu hili la msingi la ofisi hii, wadau wote wanapaswa kutoa taarifa (kwa maandishi inapobidi) zinazohusu mambo yote ya ulinzi na usalama mara baada ya vikao vya maamuzi kufanyika.

### **3.7 Kuzuia au kupunguza matukio ya uhalifu**

- (a) Menejimenti ya Chuo kupitia Ofisi ya Ulinzi na Usalama itawajibika kutoa /kuratibu utoaji wa elimu juu ya njia za kuzuia au kupunguza matukio na viashiria vya uhalifu kama vile:
  - (i) Wizi na ujambazi;
  - (ii) Mauaji au kujeruhi;
  - (iii) Uharibifu wa mali, vifaa, majengo, n.k;
  - (iv) Taarifa za moto;
  - (v) Hujuma ya mali, majengo ya Chuo;
  - (vi) Kuingia kwenye maeneo ya Chuo bila kufuata sheria;
  - (vii) Fujo/ghasia, migomo, maandamano yasiyo halali kwenye maeneo ya Chuo;
  - (viii) Namna ya kumtambua/kuwatambua wahalifu; na
  - (ix) Vitendo vingine vinavyokwenda kinyume na sheria za nchi.

- (b) Chuo kitashirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama katika kutoa elimu juu ya mambo mbalimbali yahusuyo ulinzi na usalama.
- (c) Katika kuhakikisha ulinzi binafsi na kuzuia matukio hatarishi kwa usalama binafsi, kila mwanajamii atawajibika kwa usalama wake na mali zake na kwamba atatakiwa kutoa taarifa kwa Ofisi ya Ulinzi na Usalama mara moja anapoona kuna uwepo wa vihatarishi vya usalama wake na mali zake.
- (d) Iwapo mtu yeyote atahitaji kupewa ulinzi binafsi au kusindikizwa, atalazimika kuwasiliana na Afisa Usalama angalau dakika 30 kabla ya kuhitaji huduma hiyo.

### **3.8 Utunzaji wa Funguo za Ofisi**

Ili kuhakikisha usalama wa mali zilizopo ndani ya ofisi, mambo yafuatayo kuhusu utunzaji wa funguo za ofisi yatazingatiwa:

- (a) Hakuna mfanyakazi au mwanachuo yeyote atakayeruhusiwa kwenda na funguo za ofisi au za chombo cha usafiri nyumbani au bwenini kwake au nje ya eneo la Chuo;
- (b) Funguo zote zitahifadhiwa katika kasiki maalum za utunzaji wa funguo ambazo zitakuwa katika maeneo maalum yatakayoainishwa na mamlaka za Chuo;
- (c) Mtumishi wa Chuo au mwanachuo mwenye kitambulisho tu ndiye atakayeruhusiwa kuchukua funguo za ofisi kwa watumishi na madarasa kwa Wanachuo;
- (d) Walinzi wa zamu watahakiki usahihi wa taarifa na vitambulisho, na kuandika au kurekodi namba au taarifa za vitambulisho vya wanaochukua funguo kabla na wakati wa kurudisha funguo;
- (e) Kila mfanyakazi atawajibika kufunga mlango, dirisha, kuzima taa na vifaa vyote vinavyotumia umeme kabla ya kuondoka ofisini; na

- (f) Wakati wa kurudisha funguo, mlinzi wa zamu wa mapokezi atahakikisha kwa kukagua mlango husika.

### **3.9 Matumizi ya Mawasiliano**

Ili kurahisisha ulinzi na usalama pamoja na upatikanaji wa taarifa, Chuo kitaweka mifumo mbalimbali ya usalama na mawasiliano itakayokuwa ni rafiki miongoni mwa wadau wanaohusika katika ulinzi na usalama, mfano; kamera za ulinzi, simu, barua pepe, vyombo vya usafiri, masanduku ya maoni n.k.

### **3.10 Adhabu kwa Makosa Mbalimbali**

Kutakuwa na adhabu zitakazotolewa kwa mtu yeyote atakayekiuka masharti yaliyowekwa na Mwongozo huu. Adhabu hizi zinaweza kuongezwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama au vyombo vingine vya juu kutegemeana na makosa husika. Adhabu pendekezwa ni:

- (a) Makosa yote yatakayofanywa na watumiaji wa mabweni, sheria zinazoongoza mienendo ya Wanachuo (*students by-laws*) zitatumika;
- (b) Kufanya biashara ndani ya eneo la Chuo bila kibali: Atakayepatikana na kosa hili atatozwa kuanzia TZS 50,000 hadi TZS 100,000 pamoja na kuzuiwa kupewa kibali;
- (c) Atakayekiuka masharti ya mkataba aliopewa atatozwa kuanzia TZS 50,000 hadi TZS 100,000 pamoja na kupewa onyo au kunyang'anywa kibali kutegemeana na ukubwa wa kosa lililofanyika;
- (d) Atakayekata miti kila mti utatozwa kuanzia faini ya TZS 50,000 hadi TZS 70,000 au zaidi kulingana na ukubwa wa mti na kunyang'anywa miti iliyokatwa;
- (e) Kuchunga mifugo: Mhusika atatozwa kuanzia faini ya TZS 60,000 hadi TZS 100,000 kwa idadi yoyote ya mifugo;

- (f) Kukata nyasi: Mhusika atatozwa kuanzia TZS 30,000 hadi TZS 50,000 na kunyang'anywa nyasi;
- (g) Kutupa taka katika eneo la chuo: Mhusika atatozwa faini ya kuanzia TZS 50,000 hadi TZS 200,000 na kulazimika kuziondoa taka zake katika eneo husika.
- (h) Uhalifu mwingine: Kamati ya ulinzi na usalama itaamua kwa kuzingatia Sheria za nchi.

### **3.11 Ujirani Mwema**

Ili kuwa na usalama na majirani wanaozunguka eneo la chuo, Chuo kitaweka utaratibu wa kukutana na viongozi wa mitaa inayoizunguka kwa ajili ya kujadili mambo ya ulinzi na usalama. Katika kutekeleza jambo hili, Ofisi ya Ulinzi na Usalama itaratibu yafuatayo:

- (a) Kuandaa mikutano ya ujirani mwema ili kuboresha mahusiano. Mikutano hii itafanyika kila baada ya miezi mitatu (robo mwaka);
- (b) Kutoa elimu elekezi kwa wananchi kuhusu namna bora ya kutunza miundombinu;
- (c) Kuwaomba na kuwashauri wamiliki nyumba za kupangisha watoe taarifa kwa Chuo kwa ajili ya kuboresha ulinzi na usalama kwa Wanachuo watakaopanga nyumba hizo; na
- (d) Kuandaa utaratibu kwa kushirikiana na Wenyeviti na Watendaji wa Mitaa, kuzitambua nyumba wanazoishi Wanachuo.

### **3.12 Matumizi ya Mifumo ya Kamera za Usalama (CCTV) na Usalama wa Mifumo ya Taarifa**

Mifumo ya Kamera za Usalama (CCTV) inasaidia katika kuweka usalama na kuhakikisha maeneo yanakuwa na ulinzi wa kutosha kwa kuzuia na kutunza



taarifa za uhalifu na viashiria vyake ikiwa ni pamoja na kuwezesha kuwatambua wahalifu.

- (a) Kutakuwa na mfumo wa CCTV ambazo zitawekwa katika maeneo maalum ya nje na ndani ya majengo ili kuhakikisha taarifa za matukio yanayohatarisha usalama yanadhibitiwa kwa kupata taarifa sahihi na kwa wakati.
- (b) Kutakuwa na chumba maalum kwa ajili ya kufuatilia matukio mbalimbali kila siku kupitia mfumo wa Kamera za Usalama (*CCTVs Control Room*).
- (c) Kutakuwa na utaratibu wa kutunza taarifa za kila wiki zinazopatikana katika mfumo wa Kamera za Usalama katika sehemu salama kwa ajili ya matumizi zinapohitajika.
- (d) Usalama wa kimifumo utafuatiliwa kwa kufuata miongozo ya ulinzi wa TEHAMA (*MUST ICT Security Guidelines*).

### **3.13 Ushughulikiaji wa Madawa ya Kulevya**

Katika kuhakikisha Chuo kinakuwa mahali salama, ambapo hakuna matumizi au uwepo wa madawa ya kulevya, mambo yafuatayo yatazingatiwa:

- (a) Iwapo kuna mtu yeyote mwenye taarifa za mtu au kikundi cha watu wanaolima, wanaozalisha, kuchakata, kusafirisha, kutunza au kutumia madawa ya kulevya katika eneo la Chuo atatakiwa kutoa taarifa kwa mamlaka za Chuo; na
- (b) Iwapo itabainika uwepo wa madawa au matumizi ya madawa ya kulevya kwa mtu au kikundi cha watu, uchunguzi utafanyika kwa ushirikiano kati ya Chuo na mamlaka za Serikali zinazohusika, na ikithibitishwa, hatua zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

### **3.14 Udhhibiti wa Silaha na Vifaa vya Milipuko**

Umiliki wa silaha na vifaa vya milipuko katika eneo la Chuo utazingatia sheria na taratibu za Nchi ili kuepusha uwepo wa silaha na milipuko:

- (a) Hakuna mtu au kikundi cha watu kitakachoruhusiwa kuwa na au kutumia silaha au milipuko isipokuwa kwa maafisa usalama waliokasimiwa jukumu hilo na mamlaka za Chuo au vyombo vya usalama wa Nchi; na
- (b) Kila mwanajumuiya ya Chuo atakuwa na wajibu wa kutoa taarifa kwa mamlaka za Chuo iwapo atapata taarifa za kuwepo au matumizi ya silaha au milipuko isivyo halali katika eneo la Chuo na taarifa hizo zitapelekwa kwenye vyombo vya ulinzi na usalama.

### **3.15 Udhhibiti wa Kemikali na Vifaa Vingine Vinavyoweza Kuathiri Usalama**

Katika Chuo kuna matumizi ya kemikali na vifaa mbalimbali vya kujifunzia ambavyo kwa namna moja au nyingine vinaweza kuathiri usalama wa wanajamii wa Chuo na mali zao/zake.

- (a) Kutawekwa utaratibu wa matumizi, utunzaji na utupaji wa kemikali, vifaa na mabaki ya vifaa hivyo kulingana na taratibu ili kuepusha matumizi au utupaji kimyume na maadili; na
- (b) Katika kila eneo lenye kemikali au vifaa hivyo kutakuwa na mtumishi maalum aliyepewa mafunzo kwa ajili ya hiyo.

## **4.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI**

Ufuatiliaji na tathmini ni nyenzo muhimu katika kupanga, kutekeleza na kupima matokeo ili kuboresha utendaji katika kuimarisha hali ya ulinzi na usalama. Ufuatiliaji endelevu na tathmini ya wakati wote huwezesha uwepo wa uwajibikaji kwa wadau wote wa ulinzi na usalama wa ndani na nje ya Chuo.

Mambo muhimu yatakayohusishwa yanalenga kusaidia kuongeza ufanisi katika kusimamia na kuhakikisha hali ya ulinzi na usalama inaimarika wakati wote. Mbinu zote zitakazotumika zitakuwa shirikishi ili kuhakikisha jamii nzima ya Chuo inahusishwa kikamilifu. Yafuatayo ni mambo/vipengele muhimu vitakavyozingatiwa katika ufuatiliaji na tathmini ya hali ya ulinzi na usalama:

### **4.1. Mbinu za Ufuatiliaji**

Katika kipengele hiki, mambo yafuatayo yatahusika:

#### **4.1.1. *Ufuatiliaji wenye lengo la kujua viashiria vya uvunjifu wa usalama***

Lengo la ufuatiliaji huu litakuwa kupata taarifa kutoka kwa wadau au watu wenye taarifa zinazohusu masuala ya usalama wa Chuo na jamii yake. Mambo yatakayoshughulikiwa ni:

- (a) Kutafuta taarifa za kiusalama kutoka kwa watu mbalimbali na kuzitumia ili kusaidia kuzuia viashiria na au matukio ya kiusalama katika Chuo.
- (b) Kufuatilia utendaji wa kampuni ya ulinzi iliyopewa dhamana kwa mujibu wa mkataba na kupata taarifa za utendaji wa kila siku, kila wiki na kila mwezi.

## **4.2. Vifaa vya Ufuatiliaji**

Ulinzi na Usalama katika Chuo utafuatiliwa na kutathminiwa kwa kutumia fomu zitakazojazwa na wadau mbalimbali na taarifa mbalimbali zitakazotolewa na Ofisi ya Ulinzi na Usalama na kampuni ya ulinzi.

Taarifa zote zitachambuliwa na kuchakatwa na taarifa itakayopatikana itawasilishwa rasmi kwa Kamati na Utawala wa Chuo kama mrejesho wa hali ya Ulinzi na Usalama. Aidha, mapendekezo ya Kamati pia yatawasilishwa kwa utawala kwa hatua zaidi.

**MBEYA UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY**



**MONTHLY ASSESSMENT REPORT FOR SECURITY SERVICES**

**SUMMARY ASSESSMENT FORM**

Name of Service Provider: .....

Month ..... Year .....

Assessing Office.....

**SECTION A. SERVICES PROVIDED (70% @ item 7%)**

<b>S/N</b>	<b>DESCRIPTION OF SERVICES</b>	<b>MARKS SCORED</b>	<b>REMARKS</b>
1	Services at the main gate		
2	The smartness of security guards and wearing of identity cards		
3	Services at the reception		
4	Prevention to entry of unauthorized people including children, business vendors, and other intruders		
5	Inspecting and directing visitors at the main gate and other areas		
6	Recording and preventing removal of University properties without gate pass		
7	Presence of security guards in the agreed locations		
8	Prohibiting of students, staff and visitors who are dressed indecently to enter University compounds		

9	Responding to emergencies, proper reporting and follow up on security issues		
10	Presence of firearms in the identified places		

**SECTION B. EVENTS THAT THREATEN UNIVERISTY SECURITY**

(They should concern the service provider **(30%)**)

Key: 0 events=30%, 1 event= 20%, 2 events =10% and 3+= 0%

-----

- i. -----
- ii. -----
- iii. -----

Marks (%)

Name.....Signature:..... Date.....

**TO SCORES**

A = 100 – 81      Very Good      B = 80 – 61      Good

C = 60 – 41    Average      D = 40 – 21Poor    E = 20 – 0    Very Poor

## CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA



### FOMU YA MAPUNGUFU NA MAPENDEKEZO YA MAREKEBISHO

Fomu hii inahusu mapungufu yanayobainika katika utekelezaji wa masuala mbalimbali ya kimkatiba kwa Makampuni yanayotoa huduma mbalimbali Chuoni. Fomu hii itajazwa na kutiwa saina na upande wa mtoa huduma na upande wa Chuo baada ya kukubaliana katika kikao cha tathmini ya utendaji kwamba mapungufu na marekebisho yake ni sahihi.

#### SEHEMU A.

Mapungufu yaliyobainika katika utekelezaji wa masuala ya kimkatiba wakati wa kikao cha kufanya tathmini ya utendaji

- i. ....
- ii. ....
- iii. ....
- iv. ....
- v. ....
- vi. ....

**SEHEMU B.**

Marekebisho yanayopendekezwa ili kuondoa mapungufu yaliyobainika katika sehemu A

- i. ....  
.....
- ii. ....  
.....
- iii. ....  
.....
- iv. ....  
.....
- v. ....  
.....
- vi. ....  
.....

**SEHEMU C**

Sisi tuliotia saini tunathibitisha kuwa, mapungufu yaliyobainika na mapendekezo yaliyotolewa ni sahihi katika kuboresha utendaji na utekelezaji wa masuala yaliyoainishwa katika mkataba.

Saini ya Meneja ya Mikataba wa Chuo

Saini ya Meneja wa Kampuni ya

Huduma

Jina.....

Jina.....

Saini.....

Saini.....

Tarehe.....

Tarehe.....



## **UTHIBITISHO**

Katika kikao cha 33 cha Kamati ya Ajira na Menejimenti ya Raslimaliwatu ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kilichofanyika tarehe 10 Agosti, 2023 KILIPOKEA, KUJADILI na KUIDHINISHA Mwongozo wa Ulinzi na Usalama.

Prof. Aloys N. Mvuma

**Makamu Mkuu wa Chuo**

Devota Sanga

**Katibu**